

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU

THE HANSARD

Tuesday, 26<sup>th</sup> November, 2024

*The Assembly met at the  
Main Chambers, at 2:30 p.m.*

**[Temporary Speaker (Honorable Ahmed Hamid Omar) in the Chair]**

PRAYERS

**Temporary Speaker (Ahmed Hamid Omar):** Next Order.

**Clerk-at-the-Table:** Motion.

MOTION

*REPORT OF THE STATE OF THE COUNTY ADDRESS BY THE GOVERNOR*

**MCA Bwana Mohamed Bwana (Majority Leader):** Thank you Mr Speaker.

Mr Speaker Sir, I beg to move the following Motion on the floor of the House:-

That, the terms of the House be recorded for the exposition of public policy contained in the address of the Governor delivered on Wednesday, November 20th, 2024 at 10:30 a.m.

*(Secoded)*

*(Motion Proposed)*

---

*Disclaimer: The electronic version of the Assembly Hansard Report is for information purpose only. A certified version of this Report can be obtained from the Office of the Clerk.*

*Member's Contributions*

**MCA Amina Hassan Bwanamkuu (Nominated):** Bwana Spika hata mimi nasimama kuchangia kuhusiana na hotuba ya gavana. Mheshimiwa gavana tumekuwa nae kwa haya miaka miwili na kuna maeneo mengi ambayo ameyagusa. Asilimia 70 ya wavuvi wameweza kupata fidia zao huku waliobaki wakiweza kuandikishwa. Kuna vifaa ambao wavuvi wameweza kupewa ili kuweza kuboresha uvuvi wao. kwa upande huu, wananchi wamewezwa kufurahishwa sana.

Jambo jingine ambalo limenigusa Mheshimiwa Spika, ni upande wa matibabu. Nimefurahishwa sana na gavana wetu alipozingatia na kutatua shida za wale mama waja wazito. Vifaa mbalimbali zimewezwa kupelekwa katika hospitali mbali mbali iki ziweze kusaidia katika matibabu ya wananchi. Vile vile ameweza kuajiri wahudumu ndani ya spitali kutoka maeneo tofauti ili wananchi wa saidike.

Tukiangalia upande wa ardhi, gavana ameweza kufanya mambo mengi upande huo hususan maeneo ya lamu maghribi. Baadhi ya wakaazi wameweza kupewa hatimiliki huku wengine wakiendelea kupimiwa ardhi zao. Kwa hayo machache, sina mengi bali kuomba kupitishwa kwa mswada huu.

**MCA Shekhuna Abbass Shekhuna(Mkomani) :** Asante Bwana Spika kwa fursa ili niweze kuchangia hotuba ya Gavana ya wiki iliopita. Nikitanguliza na mambo ya miundombinu, ninataka kushukuru Gavana kwa niaba ya Wodi wa Mkomani kwa upungufu wa visa vya uhalifu kwa. Hii ni kutokana na juhudi ya Gavana ya kuweka taa za barabarani kwa ndani ya muda wa miaka miwili. Napongeza na kutoa shukrani zangu kwa mheshimiwa Gavana kwa kuweza kuipa swala la usalama kipaombele ndani ya Wodi ya Mkomani.

Kwa upande wa ukulima mheshimiwa spika, tumeweza kuona katika kaunti yetu ya Lamu kwa jumla tumeweza kusaidika mbegu kama vile kunde, pojo na halikadhalika na mimi nikiwemo mmoja wa waliogawa hizo mbegu. Watu wamefaidika na wanatoa shukrani zao kwa mheshimiwa Gavana. Napongeza pia

serikali yetu ya Baraza ya Lamu kwa ushirikiano wao na serikali ya Kaunti kuletea watu wetu manufaa.

Mheshimiwa spika tumekuwa na changamoto kidogo katika Idara ya elimu. Serikali yetu ya Baraza iliopita katika mambo na elimu iliweza kuzingatia na kuweka sheria kuwa wanafunzi watakao pata alama mia tatu na zaidi wapate usaidizi bila kuwekewa vikwazo aina yeyote. Naomba mheshimiwa Gavana aweze kuzingatia mapendekezo kama haya ili jamii zetu wapate kusaidika kwa ujumla.

Jambo lingine mheshimiwa spika ni kwa niaba ya baadhi ya watu ambao kwa miaka miwili sasa bado watoto wao hawajapata ufadhili au kile tunaita basari. Watu hawa wanapata shida kwani hawajapata usaidizi kwa watoto wao wenye wako shule za upili na chuo kikuu. Tunaomba huu ujumbe iweze kufikia mheshimiwa Gavana. Sisi ni viongozi na ni jukumu letu kusaidia watu wetu ni jambo la kusikitisha katika miaka miwili na kuna watu ki kweli wanataka kusoma ni uwezo tu ndio hawana.

Vile vile mheshimiwa spika kuna wanafunzi wako katika Kaunti zingine za jirani kama vile Tana River, Mombasa, Kilifi na kaunti zingine kwa shughuli ya masomo na wanatoka Kaunti yetu ya Lamu. Ninaomba mwanafunzi yeyote mwenye hakupata msaada waweze kusaidika katika mambo na karo.

Katika upande mwingine mheshimiwa spika ni ufugaji. Wananchi wanapata usaidizi kama vile mheshimiwa Aisha anasema lakini kuna changamoto kidogo kwa upande wa madawa. Tunaomba madawa katika Wodi yangu. Wanainchi wanaomba madawa kwa sababu kuna ugonjwa wa wanyama na mifugo zinakufa.

Mheshimiwa Spika, Gavana alikuja na kutangaza kuwa kuna nafasi ya walimu idadi ya mia tatu na tano kwa walimu wa ECD. Tunaomba tupate habari kamili ili niweze kujua katika Wodi yangu niko na wangapi. Ninataka kupongeza Gavana kwa hotuba yake ya wiki iliopita na nashukuru ushirikiano wake na Baraza na pia kupongeza Baraza kwa kazi nzuri.

**ADJOURNMENT**

**[Temporary Speaker (Honorable Ahmed Hamid Omar):** Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until tomorrow Wednesday, 27<sup>th</sup> November, 2024 at 10:30 a.m.

*The Assembly rose at 4:00 p.m.*